# TAMKO LA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete**
**Rais wa Jamhuri ya**
**Muungano wa Tanzania**

Tumeamua kuzindua **KILIMO KWANZA** kama azma maalum ya kitaifa ya kuongeza kasi ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini. **KILIMO KWANZA** inajumuisha sera na mikakati inayolenga katika kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili kilimo chetu na pia kutumia fursa lukuki tulizonazo. Kwa hiyo **KILIMO KWANZA** itakuwa mhimili muhimu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na itaweka msukumo zaidi katika kufanikisha malengo yetu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Azma ya **KILIMO KWANZA** ilibuniwa chini ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ambalo ni mfumo wetu wa mashauriano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Mimi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiye Mwenyekiti wa Baraza hilo. Kikundi Kazi cha Kilimo cha 'TNBC' kilihusika na mchakato wa kubuni mkakati huo na kitakuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wake. Vikundi Kazi vingine vya 'TNBC' vikiwemo vya Ardhi, Fedha, Miundombinu na Teknolojia, Viwanda na Usindikaji, Utalii, Rasilimali Watu na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi vilitoa mchango muhimu kuhusu jinsi kila sekta itakavyochangia katika kuleta mapinduzi ya kilimo. Mchakato huu makini wa kubuni **KILIMO KWANZA** uliongozwa na Kamati ya Utendaji ya TNBC ikisaidiwa na Sekretarieti. Watu wote waliohusika katika mchakato huu wanastahili pongezi na shukrani za dhati.

Nchi yetu yenye wakazi wapatao milioni 40 imejaaliwa kuwa na hekta milioni 44 za ardhi inayofaa kwa kilimo lakini ni asilimia 23 tu ndiyo inayotumika. Kuna hekta milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na maji ya kutosha yapo lakini ni asilimia 1 tu iliyo chini ya umwagiliaji. Nchi yetu ina mifugo ya aina mbalimbali wakiwemo ng'ombe zaidi ya milioni 19, mbuzi na kondoo milioni 17. Bahati mbaya thamani ya mifugo mingi kiasi hicho haijajitokeza kibiashara na mchango wa sekta hiyo katika pato la taifa ni

mdogo mno. Aidha, Tanzania ina maziwa na mito yenye maji ya eneo la kilomita za mraba 62,000, ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi wenye urefu wa kilomita 1,424 na kilomita za mraba 223,000 za ukanda maalum wa kiuchumi baharini (Exclusive Economic Zone). Kwa kuwa rasilimali hiyo ya maji nchi yetu inaweza kuvua mamilioni ya tani za samaki lakini shughuli za uvuvi bado ni za kiwango cha chini. Nchi yetu ina rasilimali za kutosha zinazoweza kusaidia kuleta mabadiliko endelevu ya uchumi wa Tanzania na kuinua hali za maisha za wananchi. Pamoja na hayo, asilimia 34 ya Watanzania, wengi wao wakiwa wale wanaotegemea kilimo, wanaishi katika hali ya umasikini.

Kwa maendeleo ya Tanzania, kilimo ni karibu kila kitu. Hutegemewa na asilimia 80 ya Watanzania kimaisha na kinachangia asilimia 26.7 ya pato la taifa. Kinachangia asilimia 95 ya chakula kinachotumika nchini, asilimia 30 ya mauzo nje na asilimia 65 ya malighafi zinazotumika katika viwanda vyetu vya ndani. Kujitosheleza kwa chakula ni muhimu kwa usalama na utulivu wa nchi yetu pia itasaidia kupunguza mfumuko wa bei kwani chakula huchangia kiasi cha asilimia 55.9 katika kupima kiwango cha mfumuko wa bei. Kilimo ni kiungo muhimu cha sekta mbalimbali katika kuchangia kutimiza malengo ya kukuza uchumi wa taifa. Ni dhahiri kwamba hatuwezi kufuta umasikini bila kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo. Kwa jumla ili Tanzania iweze kufikia malengo yake ya maendeleo sekta ya kilimo inatakiwa ikue kutoka asilimia 4 hivi na sasa na kufikia angalau asilimia 10. Kufikia lengo hilo ndicho kiini cha dhana ya **KILIMO KWANZA** na ndiyo shabaha yake ya msingi.

Kwa kutambua umuhimu wa kilimo katika nchi yetu, kwa nyakati mbalimbali, kumefanyika jitihada maalum za kuendeleza kilimo. Miongoni mwa hizo ni pamoja na matamko kama vile Siasa ni Kilimo, Azimio la Arusha, Chakula ni Uhai na Kilimo cha Kufa na Kupona. Kutokana na jitihada hizo mafanikio ya kutia moyo yalipatikana, lakini bado hatujafikia pale tunapopatarajia pa kuwa na kilimo cha kisasa na chenye tija ya hali ya juu. Hata hivyo, tumeweza kujifunza mambo mengi ya kisera na kiutendaji ambayo yatatusaidia katika safari yetu ya kuleta mapinduzi ya kilimo katika mkakati wetu huu mpya wa **KILIMO KWANZA.**

Mpango wa kuleta mageuzi ya kilimo chetu chini ya Kilimo Kwanza unakabiliwa na changamoto nyingi. Bahati nzuri, umekuja wakati muafaka kwa kuzingatia kwamba uchumi wa dunia unapitia katika mabadiliko


makubwa yanayotoa fursa nzuri kwa maendeleo ya kilimo. Bei na mahitaji ya chakula duniani vinaongezeka mambo yanayosisitiza umuhimu kwetu kuzalisha chakula cha kutosha nchini na kupata ziada ya kuuza nje. Uwezo wetu wa kununua chakula toka nje umepungua kufuatia kupanda sana kwa bei ya chakula duniani na kutokuwepo kwa chakula cha kutosha katika masoko ya dunia. Tukizalisha ziada nasi tutanufaika na bei na mahitaji ya chakula duniani kwa sasa. Matumaini na uwezo wa kufanya hivyo tunao. Mazingira ya uwekezaji nchini yameboreshwa na ujuzi wa wakulima umeongezeka kwa hiyo tunaweza kuongeza tija na uzalishaji katika Kilimo. Pia tunayo programu kubwa ya kuendeleza kilimo (Agriculture Sector Development Programme) tunayoendelea kuitekeleza na sekta binafsi ambayo inategemewa kusukuma maendeleo ya kilimo inazidi kukua na kuimarika. Hail kadhalika, mfumo wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma nao unazidi kujengeka. Kwa hiyo kuzinduliwa kwa **KILIMO KWANZA** wakati huu kutaiwezesha Tanzania kunufaika na fursa zinazotokana na mfumo wa uchumi wa soko unaosimamiwa kwa ushirikiano kati ya sekta za umma na za binafsi.

Nguzo kuu katika kufanikisha **KILIMO KWANZA** zinahusisha kufanya mambo kadhaa. Miongoni mwake yapo yafuatayo: kukuza kilimo cha kisasa na cha kibiashara kuanzia kwa wakulima wadogo wadogo hadi wakulima wakubwa; kuweka mkakati wa muda mfupi na mrefu wa upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kilimo kwa masharti nafuu; kuboresha mipango ya ugawaji wa ardhi; kubuni sera za kuboresha mazingira ya uwekezaji pamoja na vivutio na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi. Nguzo nyingine zinahusisha utekelezaji wa programu za maendeleo ya viwanda, maendeleo ya rasilimali watu na kukuza uelewa wa matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa wakulima katika ngazi zote. Pia, kuna kuongeza matumizi ya pembejeo za kilimo na matumizi ya mitambo na mashine; upatikanaji wa pembejeo muhimu kwa wakati muafaka kwa ajili ya kuongeza mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi; kuwa na mpango madhubuti wa kuboresha miundombinu ikiwemo miradi mikubwa ya kilimo cha umwagiliaji maji, barabara za vijijini na uhifadhi bora ili kupunguza hasara baada ya mavuno. Kadhalika, lipo suala zima la kuimarisha masoko ya mazao ili mkulima apate soko la uhakika na bei zenye tija kulingana na jasho lake.

Kipimo cha mafanikio yetu kama taifa katika kufuta umasikini nchini kinategemea kilimo cha kisasa na cha kibiashara na sekta ya viwanda inayohudumia kilimo na kukuza ushindani wa Tanzania katika soko la dunia la utandawazi. Shabaha ya **KILIMO KWANZA** ni kutupeleka hatua kwa hatua katika kufanikisha malengo haya.

Katika kuleta maendeleo, changamoto kubwa si kubuni mikakati tu, bali ni usimamizi madhubuti wa utekelezaji wake. **KILIMO KWANZA** ni mwelekeo mpya katika kuleta maendeleo ya uchumi wetu ambao utekelezaji wake ni lazima uratibiwe, kusimamiwa na kufanyiwa tathmini kwa kushirikisha sekta ya umma na sekta binafsi. Hivyo basi, utekelezaji wake uwahusishe Watanzania kwa ujumla wao, uwe wa dhati na wenye kufikia malengo.

Changamoto za utekelezaji zinaweza kuonekana kuwa kubwa lakini hakuna lisilowezekana. Tuzingatie msemo wa Rais wa Kwanza na Baba wa Taifa la Tanzania Mwalimu Julius Nyerere kuwa **INAWEZEKANA TIMIZA WAJIBU WAKO.......**



**Jakaya Mrisho Kikwete**
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**3 Agosti, 2009**